Huduma ya Kristo katika Patakatifu pa Mbinguni

“Kuna hekalu mbinguni, hekalu la kweli lililojengwa na Bwana na siyo mwanadamu. Ndani yake Kristo anahudumu kwa niaba yetu, akiwezesha wamumini kufaidi manufaa ya kafara yake ya upatanisho iliyotolewa mara moja msalabani kwa ajili ya wote. Alizinduliwa kuwa Kuhani wetu Mkuu na akaanza huduma ya uombezi wakati wa kupaa kwake mbinguni. Mwaka 1844, mwishoni mwa wakati wa unabii wa siku 2,300, aliingia katika awambu ya pili na ya mwisho ya huduma ya upatanisho upatanishi. Ni kazi ya hukumu ya upelelezi ambayo ni sehemu ya mwisho ya kukomesha dhambi yote, mfano wa kutakasa patakatifu pa hekalu la Waeberania wa kale katika Siku ya Upatanisho. Katika huduma hiyo ya mfano patakatifu palitakaswa kwa damu ya kafara ya wanyama, lakini mambo ya mbinguni hutakaswa kwa kafara kamilifu ya damu ya Yesu. Hukumu ya Upelelezi hufunua kwa viumbe wa mbinguni ni nani miongoni mwa wafu wamelala mauti katika Kristo na hivyo, katika Yeye wanahesabiwa kustahili kuwa na sehemu katika ufufuo wa kwanza. Pia inadhihirisha wazi nani miongoni mwa walio hai wanaishi katika Kristo, wakitunza amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu na katika Yeye, hivyo basi wako tayari kuhamishwa kwenda katika ufalme wake wa milele. Hukumu hii huthibitisha haki ya Mungu katika kuwaokoa wale wanaoamini katika Yesu. Hutangaza kwamba wale waliodumu kuwa watiifu kwa Mungu wataupokea ufalme. Hitimisho la huduma hii ya Kristo litakuwa ndiyo mwisha wa kufungwa mlango wa rehema kwa wanadamu kabla ya Marejeo ya Yesu.” (Ebr. 8:1-5; 4:14-16; 9:11-28; 10:19-22; 1:3, 2:16, 17; Dan: 7:9-27; 8:13, 14; 9:24-27; Hes. 14:34; Eze. 4:6; Lawi: 16; Ufu. 14: 6, 7; 20:12; 14:12; 22:12)

Hekalu Mbinguni

Mungu alimwagiza Musa ajenge maskani ya duniani Mungu akae na wanadamu (Kut.25:8). Patakatifu pa awali lilitumika kwa agano la awali (kale). (Ebr.9:1). Hapa ndipo watu walifundishwa njia ya wokovu. Kama miaka 400 baadaye, Sulemani alijenga hekalu la kudumu Yerusalemu lililoondosha hema inayobebeka ya Musa (2Nyak.3:1-5:1). Nebukadreza alilliharibu hekalu hilo (2Nya.36:19), bali mateka waliorudi kutoka Babeli waliijenga (Ezr.6:14) na kupambwa na Herode Mkuu. Ndilo lililoharibiwa na Warumi mwaka 70BK. Agano Jipya hudhihirisha kwamba agano jipya nalo lina hekalu lililo mbinguni. Hili ndilo hekalu la kweli ambalo Bwana amelijenga na si mwanadamu. (Ebr. 8:1, 2). La duniani lilikuwa nakala ya hekalu halisi la mbinguni (Ebr. 9:23, 24). Katika Biblia yote, kuweko hekalu mbinguni kunajulikana (Zab. 11:4; 102:19; Mik. 1:2, 3). Yohana wa Ufunuo anakiri kuliona hekalu mbinguni (Uf. 11:19), akaona pia vifaa vya hekalu kinara (Uf.1: 12) na uvumba (Uf. 8:3), pia sanduku la agano (Uf. 11:19). Mbinguni, madhabahu ya uvumba iko mbele ya kiti cha enzi cha Mungu (Uf. 8:3; 9:13). Kwa kweli, vifaa hivyo viko kwenye hekalu la Mungu la mbinguni (Uf. 4:2; 7:15; 16:17). Hivyo kiti cha enzi cha mbinguni (Dan. 7:9, 10) kiko kwenye hekalu. Na kwa hiyo, masuala ya hukumu kutoka kwa Mungu yatafanyikia hekaluni (Uf. 15:5-8). Hivyo ni wazi kwamba maandiko yanaonyesha hekalu la mbinguni kuwa ni mahali halisi wala siyo kielelezo (Ebr. 8:2).

Huduma ya Hekalu la Mbinguni

Huduma ya Patakatifu ni ujumbe wa wokovu na Mungu ameitumia kutangaza injili (Ebr. 4:2). Huduma za hekalu la kale zilikuwa kielelezo hadi hadi kwa nyakati za sasa (Ebr. 9:9, 10). Kupitia vielelezo na desturi za hekalu Mungu alikusudia kuilekeza imani ya Israeli kwa Huduma ya Mwokozi wa ulimwengu, mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya

ulimwengu (Gal. 3:23, Yoh. 1:29). Patakatifu palionyesha hatua tatu za huduma ya Yesu: (1) kafara mbadala ya upatanisho, (2) upatisho wa kikuhani na (3) hukumu ya mwisho.

Kafara mbadala ya upatanisho: kila kafara iliyotolewa mahali patakatifu iliwakilisha Kristo aliyekufa ili mwanadamu asamehewe dhambi, akafunua ukweli kwamba pasipo kumwaga damu, hakuna ondoleo la dhambi (Ebr. 9:22). Kafara hizo zilionesha kweli zifuatazo: (1) Hukumu ya Mungu dhidi ya dhambi, kwamba mshahara wa dhambi ni mauti (Rum. 6:23) (2)Kifo cha Yesu ni badala ya kifo cha mwanadamu "ameweka juu yake maovu yetu yote (Isa.53:6; 1Kor. 15:3)(3)Mungu ndiye mtoaji wa kafara ya upatanisho (Rum. 3:24, 25; 2Kor. 5:21;). Na kwa kupigwa kwake tuliponywa (Isa. 53:5). Tofauti na kafara za zamani, Kristo ametolewa mara moja tu (Ebr. 9:26-28; 10: 10, 14). Haki ya Mungu ilitimizwa (Rum. 5:18).

Kuhani Mpatanishaji: Ikiwa kafara ndiyo iliyoondoa dhambi, kwa nini uwepo wa Kuhani ulikuwa muhimu? Uwepo wake ulionyesha hitaji la kuwapo mpatanishi baina ya mdhambi na Mungu Mtakatifu. Mpatanishi ni mmoja tu, mwanadamu Kristo Yesu (1Tim. 2:5).

1. ***Mpatanishi na kipatanisho:*** Kunyunyiza damu wakati wa huduma ya kuhani ilikuwa kuleta upatanisho (Law. 4:35). Ukuhani wa kale unadhihirisha kile Yesu akifanyacho kwenye hekalu la Mungu (Ebr. 8:1, 2). Yesu anaweza kuwaokoa kabisa wamjiao (Ebr. 7:25). Hivyo twahimizwa kumwendea kwa ujasiri (Ebr. 4:16)

2. ***Huduma katika Patakatifu:*** Inaweza ikasemwa ilijumuisha kuingilia kati, msamaha, upatanisho na kurejesha. Mdhambi anaweza kuunganishwa na Mungu (Efe. 2:18; Ebr. 4: 14-16; 7:25; 9:24; 10:19-22). Damu ya matoleo ya dhambi ilitumika kwa mojawapo ya mawili (a) ilinyunyizwa kwenye pembe za madhabahu ya uvumba (Law. 4:6, 7, 17, 18) au (b) iliwekwa pembe za madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa (Law. 4:25, 30) na kuhani aliruhusiwa kula nyama (Law. 6:25, 26, 30). Kwa yote, mdhambi aliyetubu alijua dhambi zake zimeondolewa kwake. Hivyo huduma za patakatifu zinahusiana na kuhani kumpatanisha mdhambi moja moja (Ebr. 7:25). Mdhambi anasamehewa na kuhesabiwa haki (Efe. 4:32; 1Yoh. 1:9; 2Kor. 5:21; Rum. 3:24; Luk. 10:20). Akidumisha imani kwa Yesu, mdhambi hubadilika na kuakisi tabia ya kimbingu (2Pet. 3:18; Gal. 5:22, 23). Hivyo huduma ya Patakatifu huleta kuhesabiwa haki na kutakaswa.

Hukumu ya Mwisho: Matukio ya Siku ya Upatanisho yanaonyesha hatua tatu za hukumu ya mwisho ya Mungu: (1) hukumu kabla ya miaka 1000 au hukumu ya upelelezi ambayo pia hukumu kabla ya kurejea kwa Kristo (2) Hukumu wakati wa miaka 1000 na (3) hukumu ya utekelezaji haraka baada ya miaka 1000.

1. Huduma Patakatifu pa Patakatifu: Huduma hii yahusu kutakasa hekalu na watu wa Mungu. Kwa ajili ya kutakasa hekalu, matoleo mawili yalihitajika, mbuzi kwa ajili ya Bwana na mbuzi kwa ajili ya Azazeli (Law:16:20; cf. 16:16-18. Damu ya mbuzi wa Bwana hupelekwa moja kwa moja kwenye uwepo wa Mungu yaani sanduku la agano, kwamba madai ya sheria ya Mungu yametimizwa. Mungu anayo hamu kubwa kupatanishwa na wanadamu ndiyo maana alitoa kafara ghali ya mwana wake (1Kor.5:19). Kuhani Mkuu akishafanya utakaso wa hekalu na wa watu, ndipo baadaye, akimwakilisha Kristo, huchukua dhambi zilizochafua hekalu na kuziweka kwa mbuzi anayepelekwa mbali na kambi ya watu wa Mungu. (Law. 16:16-20; 30-33).

2. ***Azazel:*** Uchunguzi makini wa mbuzi wa Azazel huhitimisha kwamba hamwakilishi Yesu. (1) kwa sababu hakuchinjwa na pasipo hakuna ondoleo la dhambi (Ebr.9:22). (2) Hekalu lilitakaswa na mbuzi wa Bwana kabla mbuzi wa Azazeli hajaingizwa (Law.16:20); Azazeli yuko kinyume na anayempinga Bwana (Law.16:8) hivyo humwakilisha vema Shetani.

3. ***Hatua tofauti za hukumu:*** (1) Kuondolewa dhambi Patakatifu huonyesha hukumu ya uchunguzi, kwa kuangalia majina yaliyoko kwenye kitabu cha uzima. (1Pet.4:17,18) (2) Kumwondosha mbuzi wa Azazeli huonyesha kifungo cha miaka 1,000 cha Shetani (Uf.20:4; 1Kor.6:1-3) na (3) Kuwa na kambi safi, huwakilisha kutakaswa kwa dunia, moto utakapoharibu dhambi na wenye dhambi (Uf.20:11-15; Mt. 25:31-46; 2Pet.3:7-13)

Wakati wa Hukumu: Wote Kristo na Baba wanaendesha hukumu ya uchunguzi. Kabla ya kuja duniani akiwa na utukufu, mwana wa Adamu alimjia Mzee wa Siku na kusimama mbele zake (Dan.7:13). Tangu Yesu alipopaa (Mdo.1:9-11), amekuwa Kuhani Mkuu akituombea (Ebr.7:15). Lakini safari hii, anakuja kupokea ufalme (Dan.7:14)

1. ***Kuyoyoma kwa Huduma ya Yesu ya Kikuhani:*** Danieli sura ya 8 hutuonyesha pambano baina ya wema na uovu, na hatimaye ushidi wa Mungu. Katika hii sura, huduma ya kikuhani inasimuliwa mwanzo wake hadi mwisho wake. Kondoo mume ni Ufalme wa Wamedi na Waajemi (Dan.8:3). Pembe zake mbili zaonyesha mamlaka mbili za Umedi na ile iliyoonekana zaidi, ni Uajemi (Dan.8:4). Beberu anayeibukia magharibi ni Ufalme wa Ugiriki na pembe yake inamwakilisha mfalme wake wa kwanza, Alexander Mkuu (Dan. 8:21). Akitokea magharibi, Alexander Mkuu aliiteka Uajemi na baadaye ufalme wa Ugiriki uligawanywa kwa majemedari wake wane, Cassander, Lysimachus, Seleucus na Ptolemy (Dan.8:8, 22). Mwisho wa Ugiriki iliyogawanyika, pembe ndogo ingekuja kuinuka (Dan.8:9). Baadhi ya wasomi wamedhani kwamba hii pembe ndogo ni Antiochus Epiphanes Mfalme wa Siria aliyetawala Palestina kwa kipindi kifupi kabla ya Yesu. Wengi, pamoja Wanamatengenezo, wanaamini huu ni ufalme wa Rumi.

   (a) Pembe ndogo ingekuwa na mamlaka tangu kuanguka ufalme wa Ugiriki hadi mwisho wa wakati, (Dan. 8:17). Ni Rumi pekee, ya kipagani na kipapa inayotimiza unabii huu.
   (b) Danieli 2, 7 na 8 zinazungumzia mamlaka za dunia zinazofanana, hivyo, tafsiri ya chuma na mnyama wa kutisha bado ni Rumi ambayo kwenye sura ya 8, inaonekana kama pembe ndogo. (Dan. 8:25; cf.Dan.2:34)
   (c) Umedi na Uajemi zilikuwa Kuu, lakini Rumi ilizidi (Dan. 8:4, 8, 9). Rumi pekee inatimiza unabii huu.
   (d) Ni Rumi iliyopanua himaya yake hadi kusini yaani Misri (Dan.8:9)
   (e) Rumi ilimpinga Mkuu wa Jeshi, ambaye ni Kristo (Dan. 8:11, 25). Rumi ya kipagani ilitaka kumwua wakati anazaliwa, na ilimsulubisha hata kuharibu hekalu lililokuwa Yerusalemu. Rumi ya Kipapa ilihafifisha huduma ya Yesu ya Ukuhani mbinguni (angalia Ebr.8:1,2). Nguvu ingekuwa kubwa na kustawi (Dan.8:12)

2. ***Wakati wa Kurejeza, Kutakasa na Hukumu:*** Mungu hakurusu kutoweka kwa ukweli wa huduma ya Kuhani Mkuu, Kristo Yesu. Katika kuelekea mwisho, huduma hii itainuliwa (Dan. 8:17) atakapoanza huduma ya upatanisho na hukumu ya upelelezi (Ebr. 7:25). Maono yanataja wazi wazi ni lini Kristo angeanza huduma hii. Hata nyakati za asubuhi elfu mbili na mia tatu ndipo Patakatifu patatakaswa (Dan. 8:14). Kwa kuwa inahusu nyakati za mwisho, haiwezekani, mambo ya hekalu yakahusu hekalu lililoko duniani kwa kuwa hilo

liliharibiwa na Warumi mwaka 70BK. Sasa kuzielewa nyakati za asubuhi na jioni 2,300 ndiyo jukumu letu la sasa. Katika unabii, siku moja, huwakilisha mwaka moja (Eze. 4: 6; Hes. 14:34). Hivyo siku 2,300 ni miaka halisi 2,300.

a) Danieli 9 inasaidia kuelewa Danieli 8: Mungu alimwagiza malaika Gabrieli kumwelewesha Danieli (Dan.8:16) lakini ilimshtua sana Danieli kwa malaika kusitisha maelezo. "Nilifadhaishwa na maono, nami sikuweza kuyaelewa" (Dan.8:27 KJV). Kwa sababu ya kuingiliwa, Malaika Gabrieli alisubiri hadi hali iwe itengemae ndipo atoe ufafanuzi (Dan.9:23). Muda wa majuma 70 umeamriwa juu ya watu wako na juu ya mji wako mtakatifu. (Dan.9:24). Kuamriwa imetafsiriwa kutoka neno la kiebrania *Chathak*. Ni neno lililotumika mara moja tu katika maandiko matakatifu. Maana yake halisi ni 'kukatwa' au 'kugawanywa'.

Majuma 70 (Miaka 490) 34BK Miaka 1,810	
+	

Kwa utangulizi huu sasa maelezo ya Malaika Gabrieli wazi. Kwamba miaka 490 ilikuwa ikatwe kutoka miaka 2,300. Mwaka wa kuanzia kuhesabu ni mwaka wa amri ya kujenga upya Yerusalemu. (Dan. 9:25) Amri ya mwisho kujenga ilitolewa na Artashasta - baada ya Koreshi na Dario mwaka 457KK (Dan.7:21 cf. 6:14). Miaka 490 ilikoma mwaka 34BK na hivyo miaka 2,300 kukoma 1844BK.

b) Kuelewa huduma ya Yesu ya Ukuhani Hekaluni Mbinguni: Mwanzoni mwa karne ya 19, wakristo wengi wakiwamo Wabaptisti, Wapresbiterian, Wamethodist, Walutheri waanglikana na Waepiskopol wajifunza unabii wa Danieli sura ya 8. Wanafunzi hawa wa Biblia walitarajia tukio muhimu baada ya mwisho wa miaka 2,300. Walitabiri huenda kukawa na kutakaswa kanisa, ukombozi wa Palestina, kuanguka kwa Ufalme wa Kituruki, kukomeshwa kwa upapa na kuisafisha dunia kwa moto na kurejea kwa Kristo kwa mara ya pili. Utabiri wao haukutimia ila maumivu yaliwapata zaidi wale waliosubiri kuja kwa Yesu mara ya pili kuliko makundi mengine. Ndipo kujifunza upya juu ya hekalu kukaanza na hekalu la mbinguni kujulikana na huduma zake kueleweka.

Umuhimu katika Pambano Kuu

***Kutukuzwa kwa tabia ya Mungu*:** Kupitia kazi ya pembe ndogo, Shetani alithubutu kupinga mamlaka ya Mungu. Matendo ya mamlaka hiyo yamehafifisha na kukanyaga hekalu la mbinguni, ambako ndiko kiti cha enzi cha Mungu kilipo. Maono ya Danieli yanaonyesha hukumu ya upelelezi ambayo Mungu atajipatia haki na pembe ndogo kuhukumiwa, kwa nuru iliyoko msalabani. Hatimaye wote, watakubali kwamba Mungu yuko sahihi, na kwamba hawajibiki kwa kuwepo dhambi ulimwenguni. Tabia yake haitabishaniwa na utawala wake wa upendo utathibitika.

Kutukuzwa kwa watu wa Mungu: Wakati hukumu inaipata mamlaka ya Pembe Ndogo, itawapa ijara njema watakatifu (Dan. 7:22). Hukumu hii haimpi Mungu utukufu peke yake ila na watu wake pia. Yeyote anayenikiri mbele za wanadamu, nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni (Mt. 10;32; Luk. 12:8,9; Uf. 3:5)

Hukumu na Wokovu: Je, hukumu ya upelelezi inahatarisha wokovu wetu? Jibu ni hapana. Tunamwamini Yesu kuwa ni mpatanishi (Rum.8:34) na tunayo ahadi kwamba tunaye mwombezi kwa Baba. (1Yoh. 2:1). Hukumu ni muhimu kwa ajili ya ulimwengu, kwamba wataruhusiwa tu wale ambao wameongoka na ndiyo maana vitabu vinafunguliwa (Dan. 7;9, 10).

Wanadamu walio hai, wako katika makundi matatu (1) waovu, ambao wamekataa mamlaka ya Mungu (2) Waumini wa kweli wanaoamini katika kile alichowatendea Yesu na kutii amri zake na (3) Wale wanaoonekana kuwa ni waumini lakini kiukweli hawako hivyo.

Malaika ambao hawakuasi wanaweza kulitambua lile kundi la kwanza. Sasa yupi ni muumini halisi na wa uwongo? Majina ya halisi na wasio halisi yote katika kitabu cha uzima. (Luk.10:20; Wafil. 4:3; Dan. 12:1; Uf. 21:27). Kanisa lina ngano na magugu (Mt. 13:28-30). Viumbe wa Mungu hawana ujuzi wote, hawawezi kusoma mioyo. Hivyo vitabu vitashuhudia wale waliokiri imani, wakaishi sawa sawa na walivyoamini na hivyo kufungua vitabu ni muhimu. Yesu alikisema kipindi hiki kwa mfano wa mtu aliyekaguliwa akakosa vazi la arusi (Mt. 22:11). Vazi hili ni tabia safi isiyo na doa ambayo waumini watakuwa nayo(Uf. 19:8; Efe. 5:27). Wale wanaodai ni wafuasi wa Mungu lakini hawakuvikwa vazi la haki ya Kristo, watafutwa kwenye kitabu cha uzima (Angalia Kut. 32:33). Haki inayokubalika ni ile iliyo ya Kristo pekee (Wafi. 3:9) na kigezo cha miujiza au unabii hakitumiki hapa (Mt. 7:21-23). Badala ya kupora waumini uhakika wa wokovu, fundisho la hekalu, huimarisha uhakika wa wokovu kwa wote wanaoutafuta kwa makini.

Wakati wa Kuwa Tayari: Mungu amekusudia kwamba hii habari ya wokovu kabla Yesu hajahitimisha huduma yake ya uombezi ienee duniani kote kabla Kristo hajerea. Ujumbe wa malaika wa kwanza unasema “mcheni Mungu na kumtukuza kwa kuwa saa ya hukumu yake imekuja (Uf. 14:7). Ujumbe huu huonya juu ya hukumu inayoendelea sasa. Kama Israeli ya zamani, tuko kwenye Siku ya Upatanisho na tunapaswa kuzitesa nafsi (Law. 23:27). Hivyo Mungu anamwita kila mwanadamu atubu katika saa hii ya hukumu (Uf. 14:7). Huduma ya Kristo inaelekea kwenye ukomo. Haijulikani ni lini Mungu atasema inatosha: “Kesheni na kuomba kwa kuwa hamjui ni lini (Mk. 13:33). Hata kama tunaishi nyakati za kutisha, hatupaswi kutishika. “Basi iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.” (Ebr.4:14-16)